TANZANIA PRIVATE SECTOR FEDERATION

# Tafakari ya TPSF kuhusu Mazungumzo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Sekta Binafsi




June, 2026

# Utangulizi: DIRA 2050 na Nafasi ya Sekta Binafsi

Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 (DIRA 2050), ulioanza tarehe 1 Julai 2026, unaashiria mwanzo wa hatua mpya katika safari ya maendeleo ya Tanzania. Dira hii inalenga kuijenga Tanzania kuwa na uchumi imara, wenye ushindani na jumuishi kwa kuimarisha uzalishaji, maendeleo ya viwanda, ubunifu na uwekezaji, kwa lengo la kufikia uchumi wa thamani ya Dola za Marekani trilioni moja ifikapo mwaka 2050.

Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) unatafsiri DIRA 2050 katika malengo na matokeo ya maendeleo yanayopimika kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Mpango huu unalenga kufikisha Pato la Taifa kwa bei za sasa hadi Dola za Marekani bilioni 118.052, kukuza Pato la Taifa kwa asilimia 10.5 kwa mwaka na kufikisha Pato la Taifa kwa kila mtu hadi Dola za Marekani 1,638 ifikapo mwaka 2031. Malengo hayo yanatarajiwa kuchochewa na ukuaji mkubwa katika sekta muhimu za uzalishaji, ikiwemo viwanda (asilimia 10.8), madini (asilimia 9.0), ujenzi (asilimia 8.5) na kilimo (asilimia 10.0). Aidha, Mpango unaweka kipaumbele katika kuimarisha sekta ya fedha kwa kuongeza mikopo kwa sekta binafsi hadi kufikia asilimia 25 ya Pato la Taifa. Serikali pia inalenga kuongeza uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa kutoka asilimia 14.9 mwaka 2024/25 hadi asilimia 20 ifikapo mwaka 2030/31, huku uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa ukitarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 13.1 hadi asilimia 18 katika kipindi hicho.

Kufikia malengo haya kutahitaji uwekezaji unaokadiriwa kufikia Shilingi trilioni 477, ambapo zaidi ya asilimia 70, sawa na takribani Shilingi trilioni 334, inatarajiwa kutoka sekta binafsi. Hali hii inaonesha nafasi muhimu ya sekta binafsi katika kuendesha mageuzi ya viwanda, kuongeza thamani ya madini, kuendeleza kilimo cha kibiashara, kukuza sekta ya fedha na kuchochea ubunifu katika uchumi kwa ujumla.

Katika muktadha huu, Mazungumzo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Sekta Binafsi ni hatua muhimu katika kuharakisha utekelezaji wa DIRA 2050. Mazungumzo hayo pia yameimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika safari ya kujenga uchumi imara, jumuishi na wenye ushindani.

# Mazungumzo ya Rais na Sekta Binafsi: Hatua Muhimu katika Utekelezaji wa DIRA 2050

| Hatua Muhimu | Umuhimu wa Kimkakati |
|---|---|
| Azimio la Pamoja kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma. | Linaweka msingi wa uwajibikaji wa pamoja kati ya Serikali na sekta binafsi. |
| Uzinduzi wa nyenzo nne za utekelezaji: Mpango wa Mtazamo wa Muda Mrefu 2026/27–2050/51; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) 2026/27–2030/31; Mfumo wa Kitaifa wa Utekelezaji na Usimamizi wa Ufanisi wa Mipango ya Maendeleo; na Mkakati wa Mawasiliano wa DIRA 2050. | Inaihamisha DIRA 2050 kutoka hatua ya malengo kwenda katika utekelezaji. |
| Dhamira ya Serikali ya kuendelea kuboresha mazingira ya biashara. | Inaimarisha imani ya sekta binafsi na kuongeza sera zilizo wazi na zinazotabirika. |
| Dhamira ya kuendeleza majadiliano. | Inaimarisha mifumo ya kitaasisi ya kuendeleza mageuzi ya sera. |

# Mtazamo wa Sekta Binafsi: Vipaumbele vya Kufanikisha DIRA 2050.

Sekta binafsi inathamini uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuandaa na kuongoza mazungumzo na sekta binafsi. Mazungumzo hayo yaliangazia maeneo ya kipaumbele yanayohitaji hatua endelevu ili kuongeza ushindani, kuvutia uwekezaji, kuongeza tija na uzalishaji, na kuhakikisha ushiriki mpana na jumuishi katika mageuzi ya uchumi wa Tanzania.

a. Kuharakisha Utekelezaji wa Mageuzi ya Kodi na Sheria: Ingawa vikwazo mbalimbali vya muda mrefu vinavyoathiri mazingira ya biashara vimebainishwa, kipaumbele cha sasa ni kuharakisha utekelezaji wa mageuzi ambayo tayari yameainishwa. Jambo la msingi ni kutekeleza mapendekezo 284 ya Tume ya Rais ya Mageuzi ya Kodi, yanayolenga kuufanya mfumo wa kodi kuwa wa kisasa zaidi, kuboresha usimamizi wa mapato na kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini Tanzania.
b. Kuweka Mazingira Wezeshi ya Kuvutia Uwekezaji wa Sekta Binafsi: Kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi wenye thamani ya Shilingi trilioni 334 katika kipindi cha miaka mitano ijayo kutahitaji mageuzi yatakayoongeza sera zilizo wazi na zinazotabirika, kupunguza gharama za udhibiti na uzingatiaji wa sheria, kupanua upatikanaji wa mikopo yenye gharama nafuu, kuimarisha mifumo ya usafirishaji na uwezeshaji biashara, kuharakisha maandalizi ya miradi inayoweza kufadhiliwa kupitia Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), pamoja na kukuza ujuzi unaoendana na mahitaji ya viwanda.
c. Kupanua Ushiriki wa Biashara za Ndani katika Fursa za Kiuchumi: Mazungumzo hayo pia yalisisitiza umuhimu wa kuongeza ushiriki wa Watanzania katika fursa za kiuchumi. Kwa mfano, takribani asilimia 2 ya wakandarasi wa kigeni wanapata zaidi ya asilimia 70 ya thamani ya mikataba yote ya ujenzi wa umma. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuimarisha uwezo na ushindani wa wakandarasi wa ndani, pamoja na kuwawezesha kupata masoko na fursa zaidi za biashara.
d. Kuharakisha Mageuzi ya Kidijitali na Matumizi ya Akili Unde (AI) ili Kuongeza Ushindani: Kuongeza matumizi ya Akili Unde (AI), teknolojia za kidijitali na ubunifu ni muhimu katika kuongeza tija na uzalishaji, kupunguza gharama za uendeshaji na kuziwezesha biashara, hususan biashara ndogo na za kati (MSMEs), kushindana kwa ufanisi katika uchumi wa dunia unaozidi kutawaliwa na teknolojia za kidijitali.
e. Kuimarisha Utekelezaji, Ufuatiliaji na Uwajibikaji: Utekelezaji wa mageuzi unapaswa kuungwa mkono na mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na uwajibikaji. Kuweka utaratibu wa kudumu wa Mazungumzo kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPD) kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), mazungumzo ya kisekta katika wizara, pamoja na mabaraza ya biashara ya mikoa na wilaya, sambamba na ufuatiliaji wa kimfumo wa utekelezaji wa mageuzi yaliyokubaliwa, kutaimarisha uwajibikaji, kudumisha imani ya wawekezaji na kuhakikisha kuwa ahadi zinaleta matokeo halisi ya kiuchumi.

# Matokeo ya Awali ya Mazungumzo ya Rais na Sekta Binafsi

Mazungumzo hayo yalibainisha hatua kadhaa za kisera zilizotolewa ufafanuzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambazo zinaweza kuchochea na kuharakisha utekelezaji wa DIRA 2050:

i. Fursa Zaidi kwa Wakandarasi wa Ndani: Mhe. Rais alieleza kuwa mageuzi ya hivi karibuni ya sera yataongeza fursa za kampuni za ndani kupata mikataba ya umma. Aidha, wakandarasi wa kigeni watahimizwa kuingia katika ubia na kampuni za Kitanzania. Wakandarasi wa ndani pia wamehimizwa kuendelea kujenga uwezo na kuimarisha ushindani wao.

ii. Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Miundombinu ya Viwanja vya Ndege: Mhe. Rais aliihimiza sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu ya viwanja vya ndege, hatua inayoonesha dhamira ya Serikali ya kupanua ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa miundombinu ya kimkakati chini ya DIRA 2050.

iii. Kuanzishwa kwa Soko la Kimataifa la Madini: Mhe. Rais alipokea pendekezo la kuanzisha soko la kimataifa la madini na kueleza kuwa Serikali italifanyia kazi kwa kuchunguza uwezekano wa utekelezaji wake. Soko hilo linaweza kuwa nyenzo muhimu ya kupanua fursa za masoko na kuimarisha uongezaji thamani katika sekta ya madini.

# Hitimisho

TPSF inaendelea kudhamiria kuunga mkono mazungumzo ya mara kwa mara na yenye utaratibu kati ya Serikali na sekta binafsi, kuratibu vipaumbele vya sekta binafsi, na kushirikiana na Serikali pamoja na wadau wengine katika kujenga mazingira wezeshi kwa uwekezaji, ushindani na ukuaji endelevu wa uchumi, tunapoendelea na utekelezaji wa DIRA 2050.